Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 81 No. 220 | RAJ. - SHAB. 1442 AH | MACHI 2021 | AMMAN 1400 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

(Hao ndio) wanaotubu, wanaoabudu, wanaotukuza, wanaofunga saumu, wanaorukuu, wanaosujudu, wanaoamuru yaliyo mema, na wanaozuia yaliyo mabaya, na wanaohifadhi mipaka ya Allah - na wape habari njema waaminio.
(AT-TAUBA 9:112)

Siku ya Masihi Aliyeahidiwa as

Na **Al-Ustadh Issa Malenge**
Kitunda, Dar es salaam

Sawa na kalenda ya Jamaat Ahmadiyya tarehe 23/3 kila mwaka ni siku ya Maadhimisho ya Masihi Aliyeahidiwa.

Hivyo ningependa kuwakumbusha baadhi ya mambo muhimu yanayo husiana na siku hii muhimu.

Siku kama ya leo Jamaat Ahmadiyya ilianzishwa na Hadhrat Ahmad a.s. kwa amri ya Allah ilikua ni tarehe 23/03/1889.

Sayidna Mirza Ghulamu Ahmad a.s. alizaliwa tarehe 13/02/1835 huko Qadian India .

Alijitolea maisha yake yote kujifunza elimu ya Quran tukufu na kumwabudu Allah.

Kwa kuona hali duni ya Waislaam na kushambuliwa sana na wapinzani, alimwomba Allah kwa unyenyekevu sana kwa ajili ya mafanikio ya Islaam.

Vile vile alijitahidi kujibu shutuma za wapinzani na kutetea dini ya kweli.

Allah alimchagua kua Imamu wa zama hizi, hivyo alifanya kazi ya kuielezea dunia juu ya mafundisho sahihi ya Islaam.

Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w. ndiye Mwalimu kamili ambaye ametuelezea mambo yote yatakayotokea mpaka siku ya Kiyama.



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad as
Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi

Kwa idhini ya Allah, alituelezea vizuri hatari ya mifarakano katika Dini ya Kiislamu na dawa yake.

Sahaba mmoja Hadhrat Huzaifa Bin Yaman R.A anasimulia kwamba nilimuuliza Mtume Mtukufu s.a.w. kwamba tulikuwa katika upotevu na giza mpaka Allah alikutuma.

Sasa tumepata mwongozo na nuru. Je baada ya hayo tena tutapotea?

Mtume Mtukufu s.a.w. alijibu ndiyo.

Nilimuomba atueleze zaidi kuhusu upotevu huu.

Alieleza kwamba wafalme wabaya watatawala, Waislamu watagawanyika, viongozi wao wataongoza kinyume na mwongozo wangu na watafundisha kinyume cha suna zangu. watakuwa mashetani katika mavazi yetu (ya Kiislamu), wale watakaowaitikia watatupwa motoni.

Nilimuuliza Mtume s.a.w. unatuamuru nini katika hali hii? Alisema (katika hali hiyo) jiungeni na Jumuiya ya Waislamu yenye Imam mmoja.

Nilimuuliza tena kwamba kama haitakuwapo Jumuiya wala

Endelea uk. 3

Msikiti Wafunguliwa Tawi la Chanika

Na **Mwandishi Wetu**
Chanika, Dar es salaam

Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Wailsam wa Ahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry sahib aliwaongoza wanajamaat wa Dar es Salaam na mikoa ya Jirani katika hafla ya ufunguzi wa Msikiti mpya uliopo Chanika unaoitwa Masjid Mahd.

Kwa fadhila za Allah Jamaat Ahmadiyya nchini Tanzania imekuwa ikipiga hatua kila kukicha na kupanua wigo wa kutoa huduma za kiroho na kimwili kwa binadamu na safari hii katika Mkoa wa Dar es Salaam



Msikiti mpya uliopo katika tawi la Chanika

ulianza ujenzi na kumalizika kwenye tawi la Chanika lililopo katika Manispaa ya Jiji la Ilala ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam limefanikiwa kupata msikiti na kufunguliwa rasmi tarehe ishirini na nane mwezi wa pili mwaka wa 2021.

Hafla hiyo ilianza mara baada ya Sala ya adhuhuri kwa kufanya maombi ya kimya ya ufunguzi rasmi wa msikiti huo yaliyoongozwa na Amiri na Mbashiri Mkuu. Baadaye ikafuata ratiba ya shughuli hiyo kwa ufunguzi kwa usomaji wa Qur'an Tukufu iliyosomwa na Hafidh

Endelea uk. 2

Tiba ya Mwili na Roho? uk. 5

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

JE WAISLAMU WANAWEZA KUWA SEHEMU YA NCHI ZA MAGHARIBI

"Ni jambo linalonipa furaha sana kuwa Waahmadiyya sio watu wanaojiweka kando katika jamii wanamoishi bali wanafanya kila njia kuwa pete na kidole na jamii ile wanamoishi kwa hakika hiyo ni alama ya kila Ahmadiyya wa kweli."

Hayo ni maneno ya kiongozi mpendwa, Khalifatul Masih wa V ambaye ni kiongozi wa Jumuiya ya Ahmadiyya duniani inayopatikana katika nchi 202 na wafuasi mamilioni katika nchi hizo. Huo ni ujumbe ambao Huzur amekuwa akiueneza katika hotuba zake zote, akisisitiza kuwa mafundisho hayo yanatokana na dini tukufu ya Islam na mfano wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w.

Waahmadiyya sio tu kwamba wamesikiliza ujumbe huo wa Huzur la hasha, hatua bayana zimechukuliwa za kutekeleza maagizo hayo. Magazeti mengi ya Magharibi yameshuhudia kuwa Waahmadiyya ni mfano wa kuigwa wa jinsi gani wageni wanaweza kwa haraka kuwa sehemu ya jamii. Bila shaka maagizo haya hayapokelewi vizuri na wale wanaojiita viongozi wa Waislamu na kuwahimiza wafuasi wao wasiwe sehemu ya jamii. Suala la kujiuliza imekuaje Waahmadiyya wamefaulu kuwa sehemu ya jamii na wengine wameshindwa? Ilielezwa na Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. kuwa kutafika kipindi mafundisho yote ya Islam yatapotea, misikiti itakuwa mikubwa na mizuri bali isiyo na mwongozo, Kuran Tukufu itabaki maneno lakini bila kufahamu maana za ndani za kitabu hicho cha Allah. Lakini ilielezwa katika vitabu vingi vya dini kuwa atadhihiri Masihi atayerejesha mafundisho safi. Kazi hii amepewa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ambayo ameifanya kwa ufaulu mkubwa sana. Ni mafundisho aliyoyapata yanayoeleza maana za ndani za Kuran Tukufu yanayafanya Waahmadiyya wawe wepesi kuwa sehemu ya jamii wanapokwenda kuishi.

Hakuna tatizo linaloweza kumkabidhi Muislam akifuata mafundisho ya Kuran Tukufu na mfano wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. kwani tumekumbushwa, "Kwa hakika mnao mfano mwema katika Mtume wa Allah"

Msikiti Wafunguliwa Tawi la Chanika



Amir na Mbashiri Mkuu, Sh. Tahir Mahmood Chaudhry akifungua msikiti

Kutoka uk. 1

Lundo, Shairi maridhawa likafuata lilisomwa na Jalaludin Mbawala. Amir Jamaat ambaye alikuwa ndiye Mwenyekiti wa hafla hiyo alimtaka Rais wa tawi Dr. Swaleh Kitabu Pazi atoe salamu za tawi.

Rais wa tawi alianza kwa kumshukuru Allah kwa kutuwezesha kupata wasaa kukutana katika siku hiyo, pia alimshukuru Khalifa wa zama Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) kwa kutoa wazo la ujenzi wa msikiti wa aina hii Tanzania. Pia alimshukuru Amir Jamaat Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry kwa kupendekeza ujenzi wa msikiti huo ujengwe tawi la Chanika, kwani alikuwa na fursa ya kuchagua eneo lolote ila kipekee alipendekeza ujengwe tawi la Chanika, uamuzi huu tunaona ni hatua muhimu ya maendeleo ya Jamaat katika Jiji la Ilala, ambao ni wa kwanza kufunguliwa katika Jiji hili. Historia imeandikwa.

Rais pia aliwashukuru wageni waalikwa katika hafla hiyo, Viongozi wa Serikali ya mtaa Walioongozwa na Bwana Salum Kondo Simba, Alikuwepo mtu maarufu wa eneo hilo Mzee Mwagu, Maimamu wa msikiti wa Al Huda na Fii Sabilillah iliyopo Jirani na eneo hilo pia walikuwepo. Mialiko ilifika pia kwa viongozi wa makanisa yaliyopo Jirani alisema Rais wa Tawi.

Akitoa takwimu alisema idadi ya wanatawi inakaribia watu sitini na kueleza msikiti huo utakuwa chachu muhimu kwa mahubiri ili kuongeza wauminini na kutumia msikiti kuwa kituo muhimu kwa watu wa dini zote kwani hiyo ndiyo kazi ya msikiti. Alimalizia Rais wa tawi.

Akitoa nasaha katika hafla hiyo, Amir na Mbashiri Mkuu aliwataka wanatawi kutumia msikiti huo vizuri na kuutunza na pia kuwakaribisha watu wengine pia. Kwani wakati wa Mtume Muhammad*saw* aliwahi kuwakaribisha Wakristo kusali msikiti. Hali hii inaonyesha upendo na amani na inabidi vidumishwe katika zama hizi na hiyo ndiyo kazi ya msikiti, Alisema Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry.

Katika hafla hiyo pia walihudhuria Naib Amir, Ndugu Issa Mwakitalima, Katibu Mkuu msaidizi wa Jamaat Ahmadiyya Sheikh Abdulrahman Mohamed Amme, Sheikh wa Mkoa Jamaat Ahmadiyya Morogoro, Sheikh Asif Mahmood Butt, Mkuu wa Chuo cha Jamia Morogoro, Sheikh Abid Mahmood Bhatti Aidha alikuwepo mwenyeji ambaye ni Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Sheikh Nadeem Ahmad na Masheikh wengine toka ofisi ya Amir Sahib, Sheikh Shahab Ahmad na Sheikh Asif Raza majirani toka matawi ya Kitonga na Kivule yalioongozwa na Mwalimu Ally na viongozi wa Majlis Amila ya Ansarullah waliiongozwa na Sadr Majlis, Ally Hamis Mbambwa Sahib. Aidha Mfanyabiashara Yahya Kambaulaya Sahib ambaye alikuwepo toka hatua za uwekaji wa jiwe la msingi pia alishiriki katika hafla ya ufunguzi.

Wageni waalikwa walipata fursa ya kueleza machache na kuonyesha kushukuru kwao kwa mualiko huo ambao unadumisha udugu na ujirani mwema miongoni mwetu. Waliahidi kutoa ushirikiano wakati wowote kwa shughuli za msikiti huo.

Hafla hii ilifungwa kwa maombi ya kimya yalioongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry na baadaye kufuatiwa na dhifa iliyoandaliwa nyumbani kwa Rais wa tawi.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Ahmad Abdul Nasibu.
Mchapishaji: Sheikh Bashart Ur Rehman
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Siku ya Masihi Aliyeahidiwa as

Kutoka uk. 1



Na **Al-Ustadh Issa Malenge**
Kitunda, Dar es salaam

Imam, tufanye nini?

Alisema wacheni makundi na firka zote, na msijiunge mahali popote. Afadhali kuenda porini na kushika mizizi ya miti kwa meno mpaka kifo. (Bukhari Kitabul Manaaqib. Mishkaat Baabul Fitan).

Sasa alama zote za upotevu zimetimia. Waislamu wamegawanyika. Kweli kweli mambo yanafundishwa kinyume cha muongozo na suna za Mtume Mtukufu s.a.w. Katika hali hii amri ya Mtume Muhammad s.a.w. ni hii kwamba tujiunge na Jumuiya ya Waislamu yenye Imam mmoja.

Kwa kweli katika siku hizi makundi ya Waislamu ni mengi lakini kundi lolote halina Imam kati yao kutoka kwa Allah. Yaani ni magawanyiko tu, hakuna Jumuiya yoyote.

Kwa sababu Jumuiya inahitaji Imam na bila Imam hawaitwi Jumuiya.

Kwa fadhili ya Allah Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya inayo Imam mmoja - Khalifa kutoka kwa Allah ambaye anaongoza Waahmadiyya wa duniani kote, na ndiyo Jumuiya pekee yenye sifa hii.

Sisi tumefuata amri ya Mtume Mtukufu s.a.w.

Tumejiunga chini ya Imam na kwa sababu hii tunaitwa Jumuiya.

Tunawakaribisha wengine wote katika Jumuiya ya Waislamu yenye Imam mmoja kati yao.

Lakini kama hamtosheki na Jumuiya hii na Imam wake ilhali mnakosa Imam kutoka kwa Allah kati yenu, basi fuateni amri ya pili ya Mtume s.a.w. ya kuacha makundi yote na kwenda porini kushika mizizi kwa meno mpaka mauti yawafikie.

Hii inamaanisha kwamba watu bila Imam hawana ruhusa kujiunga na kundi lolote la dini bali wajitenge na yote kwa kiasi hiki kwamba waishi porini na wafunge midomo yao kuhusu mambo ya dini.

Hawana ruhusa wala madaraka ya kuielezea dini kwa sababu ya kukosa Imam kati yao.

Siku hizi duniani kote ni Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya pekee iliyo na Imam na Khalifa kutoka kwa Allah.

Kwa njia hii siku hizi duniani kote Waahmadiyya pekee ndio wanaostahiki kuitwa Jumuiya ya Waislamu yenye Imam mmoja na ndio pekee wanaoruhusiwa kufanya kazi ya kuwaita watu kwa Allah.

Kwa sababu hii tunawakaribisheni nyote katika Jumuiya ya Allah, ili tujenge na tupate umoja na udugu katika Dini ya Kiislamu.

Tuachane na makundi bali tutulie chini ya bendera ya Mtume Muhammad a.s.w. ambaye ni Mtume wa walimwengu.

Bendera ya Mtume Muhammad s.a.w. leo imeshikwa na mwanafunzi wake mtiifu Masihi Aliyeahidiwa - #Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s.

Mnamo mwaka 1888 mwanzoni Sayidna Ahmad a.s. alipokea amri kutoka kwa Allah ya kwamba aanze kuchukia baiati. Maneno ya agizo hilo yalikua ni haya:

إِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ واصْنَعِ الْفُلْكَ بِأَعْيُنِنَا وَوَحْيِنَا الَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ اللَّهَ يَدُ اللَّهِ فَوْقَ أَيْدِيهِمْ

Yaani, ufungapo nia basi mtegemee Allah. Na utengeneze safina mbele ya macho yetu na kwa kulingana na wahyi wetu. Wale watu watakao fanya baiat kwa mkono wako, basi mkono wa Allah utakua juu ya mikono yao.

Mnamo tarehe 1 mwezi wa 12 mwaka 1888 Hadrat Masih Mauud a.s. akatoa wito kwamba kabla ya kufanya baiat kwanza ni lazima kufanya maombi na Istikhara sawa na sunna ya Mtume s.a.w.

Baada ya kutoa tangazo hilo alisafiri kutoka Qadian mpaka Ludhiana na hapo alifikia nyumbani kwa Hadhrat Sufi Ahmad Jan.

Akiwa huko Ludhiana alitoa tangazo lingine akielezea shabaha na makusudio ya baiati kwamba:

Mpango huu wa kuchukua baiat ndio tu kwa shabaha ya kuwakusanya wacha Mungu katika Jumuiyya ili kundi kubwa kama hili la wacha Mungu liitilie dunia athari yake njema, na umoja wao uwe chimbuko la baraka na taadhima na matokeo mema kwa ajili ya Islaam . Na kwa baraka ya kuafikiana juu ya neno moja waweze kutumika kwa haraka katika huduma tukufu za kiislaam na wasiwe Waislaam wavivu na wabakhili wasio faa....

Bali wawe wenye huruma kwa watu kiasi hiki kwamba wawe kimbilio la masikini, wawe kama ma baba kwa mayatima na wawe tayari kujitoa kama yule aliye hemewa na mapenzi katika kuuhudumia Uislaam, na wafanye juhudi yote kwa ajili ya jambo hili .....

Allah akataka kuanzisha kundi hili na kulipatia mafanikio kwa ajili ya kudhihirisha ujalali wake na kuonyesha kudra yake ili aeneze duniani mapenzi ya Allah, toba ya kweli, utakaso, wema wa kweli, amani, suluhu na amani kwa binadamu.

Hivyo kundi hili litakua kundi lake makhusus naye atawapa nguvu kwa roho yake na atawatakasa na maisha machafu na ataleta mabadiliko matakatifu katika maisha yao.

Atalikuza sana kundi hili na atawaingiza ndani yake maelfu ya wakweli.

Mwenyewe atalilea kundi hili na kulistawisha kiasi ya kwamba wingi wao na baraka zao zitastaajabisha macho. Na wataeneza nuru yao bande zote nne za dunia kama ile taa iliyowekwa mahali pa juu. Nao watakua kama mfano wa baraka za kiislaamu.

Atawapa wafuasi kamili wa jumuiyya hii ushindi juu ya watu wa silsila nyingine katika baraka za kila aina.

Na daima hadi kiama wataendelea kupatikana watu miongoni mwao watakao pewa msaada na ukubalifu.

Mola huyu jalali ametaka hivyo yu mweza, hufanya atakacho.

Kila nguvu na kudra anayo yeye.

Ndani ya tangazo hilo alitoa maagizo kwamba watu watakao fanya baiat wawasili Ludhiana baada ya tarehe 20/03/1889.

(Majmu'a Ishtiharaat, J.1

Akiwa hapo Ludhiana katika mtaa wa Jadid katika nyumba ya Bwana Sufi Ahmad Jan baiat ya kwanza ilichukuliwa.

Ilikua ni tarehe 23/03/1889 sawa na riwaya ya Hadhrat Munshi Abdullah Sonari, daftari lilitayarishwa kwa ajili ya kuweka kumbukumbu za kihistoria za baiat iliyoitwa 'Baiati Toba Barae Taqwa wa Taharat' yaani baiati ya toba kwa ajili ya kupata uchamungu na utakaso.

Mtu mmoja mmoja alikua akiitwa na kufanya baiat na mtu wa kwanza kufanya baiat alikua Hadhrat Maulana Nurdin r.a.

Akitoa nasaha kwa wafanyao baiat alisema:

Baada ya kuingia ndani ya Jamaat hii yapasa kuleta mabadiliko katika maisha ya kwanza, yavkwamba iwe Imani ya kweli juu ya Allah nayo isaidie katika kila msiba. Tena yasipuuzwe maagizo yake , bali kila amri yake iheshimiwe na ithibitishwe kwa kitendo taadhima hiyo.....

Tazameni ninyi mliofanya baiat na kukiri wakati huu , ni rahisi kusema hayo kwa mdomo lakini ni vigumu kuyatekeleza, kwa sababu shetani hujishughulisha katika juhudi ya kumfanya mwanadamu asijali dini.

Humuonyesha kwamba ni rahisi kuipata dunia na manufaa yake na dini kua ni kitu cha mbali.

Kama mnataka kumridhisha Allah mjiweke tayari kwa juhudi na jitihada kwa kutimiza ahadi hii ya kuepukana na dhambi.

Msiseme neno lolote la fitina.

Msieneze shari.

Fanyeni subra mtukanwapo.

Msishindane na yeyote na hata yule anayeshindana nanyi mtendeeni kwa upole na wema.

Onyesheni mfano bora wa maongezi mazuri.

Tiini kila agizo kwa moyo mkunjufu ili Allah aridhike na hata adui afahamu kwamba mtu huyu baada ya kufanya baiati amekua tofauti na alivyokua awali.

Toeni ushahidi wa kweli kwenye kesi.

Aunganaye na Jumuiyya hii anapaswa ashikamane na ukweli kwa moyo wote, nguvu zote na roho yote.

Dhikre Habib uk 436.

Ndugu zangu wapendwa tunapo ikumbuka siku hii ya leo ya tarehe 23 mwezi wa 3 bila shaka tunapaswa kurejea tena juu ya shabaha hasa ya sisi kufanya baiat ya Masihi aliyeahidiwa.

Ni matumaini yangu tumejifunza na kujikumbusha mengi katika nukuu hizi chache.

Allah awe pamoja nanyi na neno la mwisho ni;

Sifa zote njema ni Allah.

● ***Al-Ustadh Issa Malenge, ni Mwalim wa Jamaat ambaye amewahi kuhudumia jamaat za Burundi, Kagera, Kigoma na hivi sasa anaongoza kanda ya Kitunda, Dar es salaam.***

UNAPATAJE PESA? Tajiri Mkuu ni Mteja



Na **Mtaalamu Wetu Mtandaoni**

Anayejiuliza ninawezaje kupata pesa ikiwa sina pesa...? Hana tofauti na yule anayejiuliza ninawezaje kupata mafanikio makubwa ili hali sina bahati...?
Wakati mwingine watakwambia bahati ni zaidi ya juhudi... wewe waambie bahati huwa inatengenezwa haiji kama upepo.(Bahati huwafuata wale waliotengenezea njia kuelekea kwao).
Mwenye bahati si yule aliyeokota fuko la hela njiani mwenye bahati ni yule mwenye juhudi na uwezo wa kuivuta pesa ya yule aliyeikota na kuihamishia kwake..juhudi huivuta bahati lakini bahati haijawahi kuivuta juhudi...
Pesa iko kwa watu haiko benki wala ATM, hujui kama pesa unazokopa benki zimewekwa na watu...? kazi ya benki ni kutunza pesa za watu...na kazi ya biashara ni kuhakikisha inavuta pesa za watu kupeleka kwa mfanyabiashara...

Ili kutengeneza pesa hutakiwi kuwa na pesa unatakiwa kujua ni kwa vipi watu watakupa pesa zao. Na siku zote watu huwa hawawapi pesa watu wasiowaamini...(Capital isn›t scarce; vision is....)
Hivyo usiishie tu kulalamika kwamba watu wameshindwa kukupa mtaji je, ulishawahi kujiuliza ni kwanini watu wakupe mtaji...? Ukiweza kujibu ni kwanini watu wakupe pesa zao utakuwa umejua ni kwanini wanasema huitaji pesa kupata pesa...
Unawaza kukopa ili kupata fedha za mtaji...ila hujawahi kujiuliza kama una sifa za kukopesheka... ukiwa hata na sifa moja tu ya kukopesheka basi jua unaaminika na ukiaminika unapata mtaji...
Na ukipata mtaji tambua yule aliyekukopesha amekuamini... na ukiaminiwa hakikisha huwaangushi wanaokupa pesa zao kwa maana wamekuamini kuwa wewe unaweza kutumia vizuri zaidi kuliko wao...

Watu wakiamini huduma yako wamekuamini wewe, na watu wakiiamini bidhaa yako wamekuamini wewe...ila ukiona watu wanakuamini wewe lakini hawaamini bidhaa yako au huduma yako jua kuna shida mahali...
Kila siku iendayo kwa Mungu tunampa pesa zetu Bakheresa si kwa sababu sisi ni matajiri kuliko yeye bali tunaamini yeye anaweza kuzitunza zaidi kuliko sisi...na yeye kazi yake kubwa ni kuhakikisha anazitunza vyema pesa zetu kwa kuongeza huduma bora na bidhaa bora...
Hakikisha watu wanakuamini maana wao ndiyo wameshika pesa...na kwa bahati mbaya sana watu huwa hawapeleki pesa kwa watu ambao hawawaamini... wasipokuamini wewe basi waiamini bidhaa yako au huduma yako...
Kwa maana ni kazi rahisi watu kuiamini huduma yako kuliko kumuamini mtoa huduma...ni rahisi zaidi watu kukupa pesa kuliko kuwashawishi watu waiamini idea yako ya biashara...
Usishawishike kirahisi kwamba Tunguli na hirizi vinaleta pesa, kama ingelikuwa hivyo basi dunia ingekuwa imejaa waganga wengi mabilionea...bidhaa bora, huduma bora, ufanisi na ueredi mahali ulipoajiriwa huwavuta watu kukupa pesa zao...

«There is only one boss. The customer. And he can fire everybody in the company from the chairman on down, simply by spending his money somewhere else....Spending money is much more difficult than making money...»



Kwa Heri!

Sheikh Bashart-ur-Rehman alikuwa Msimamizi wa kiwanda cha uchapaji cha Ahmadiyya Printing Press kwa miaka kadhaa akitokea katika usimamizi wa mkoa wa Dodoma kama Mbashiri wa mkoa.
Hivi sasa amerejea Pakistan ambapo amepewa majukumu mengine.
Tunamuombea kwamba Allah Apokee jitihada zake na Amjaalie mafanikio katika utumishi wa Islam Ahmadiyya huko alikopangiwa, Amin



Karibu!

Tunamkaribisha Sheikh Raghib Zial-ul-haq aliyekuja kutoka Ghana kukihudumia kiwanda chetu cha uchapaji cha Ahmadiyya Printing Press kilichopo Temeke.
Tunamtakia ufanisi, utendaji mwema na kheri nyingi katika kukipeleka mbele kiwanda chetu na kukiongezea tija zaidi.

Karibu Tanzania!

Kaondoka Bwana Ubwa

Na Mahmood Hamsin Mubiru
Kiwalani, DSM

Imenichukua muda kupata neno moja tamu la kumuelezea Bwana Hemedi Sheikh Ubwa. Hatimaye nimelipata, la Mfanyakazi huyo wa Benki ya Taifa, Mkaguzi wa Mahesabu ya Jamaat, fundi wa kuchagua maneno, aliyebeba tabasamu na kuwa na mapenzi makubwa ya kusoma, neno linaloweza kumtendea haki ni neno Muungwana. Bwana Ubwa alikuwa Muungwana. Kuondoka kwake kumetupunguzia idadi ya waungwana nchini. La kufanya hakuna ila kukubali ya kuwa kila nafsi itaonja mauti na kuwa hakika sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.



Bwana Hemedi Sheikh Ubwa (wa pili kulia) katika mashindano ya kuvuta kamba katika Ijtimaa ya Ansarullah Disemba 2020

Mwalim Ali Seba Masamba ndiye alinifanya nimuelewe vizuri Bwana Hemedi Sheikh Ubwa. Kumbe alikuwa na maradhi makubwa ya kupenda kusoma. Hapo ndipo kufahamiana zaidi kulipoanza. Mwalimu Masamba alinieleza kuwa aliwahi kuishi na Bwana Ubwa huko Muheza. Mwalimu Masamba alikuwa katika shughuli zake za biashara na bwana Ubwa alikuwa tawi la benki ya NBC la Muheza. Kilichomvutia Mwalimu Masamba ni maktaba iliyokuwa nyumbani kwa bwana Ubwa. Alijikusanyia vitabu vingi na Mwalimu Masamba alinieleza kuwa juzu zote za *Sahihi Bukhari* alikuwa nazo naye alizisomea pale nyumbani kwa bwana Ubwa. Walipata fursa ya kubadilishana mawazo ndipo hapo Mwalimu Masamba alipogundua kuwa bwana Ubwa alikuwa msomaji mzuri wa vitabu.

Haikunichukua muda na mimi kuligundua hilo. Kila tulipokutana tulipenda kunukuu ubeti wa mchezo maarufu wa William Shakespeare, *Macbeth*. La kufurahisha ni kwamba tuliweza kunukuu sawa na hali ilivyokuwa inajitokeza, kwa mathalani ilipotokea hali ya mtu unayemuamini akavunja ile imani uliyompa basi mmoja atasema:

There is no art to find the mind construction in the face.
He was a man whom I had built absolute trust. (Hii si tafsiri rasmi)

Hakuna njia ya kufahamu fikra za mtu kwa kumtizama usoni. Alikuwa ni mtu niliyemuamini sana.

Tulipofiwa na tulipokutana tukakumbushana:

Out! Out! Brief candle.
Life is but a walking shadow.
A poor player who frets his hour upon the stage.
Then he is heard no more.
It is a tale told by an idiot.
Full of sound and fury signifying nothing.

Zimika! Zimika! Ewe mshumaa mdogo.
Mimi si chochote isipokuwa kivuli kinachotembea.
Muigizaji anayetembea jukwaani.
Halafu haonekani tena.
Inabaki hadithi ya hayawani.
Iliyojaa upuuzi isiyo na maana yoyote.

(Hii si tafsiri rasmi)

Kila alipopata kitabu kipya alipenda na mimi nikipitie. Shauku yake ya vitabu nilivyoandika ilikuwa ni kubw na tulikuwa tunavipitia na ananipa ushauri.

Bwana Ubwa ametumia kalamu yake katika kueneza ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa as. *Mapenzi ya Mungu* ilikuwa inapambwa mara kwa mara na makala zake.

Itaendelea toleo Lijalo

Tiba ya Mwili na Roho

Na Mahmood Hamsin Mubiru
Kiwalani, DSM

"Ninapokuwa Muhimbili ninatibu mwili, nyumba muhimu ya roho, na ninapokuwa Kariakoo nimebeba kikapu kilichojaa dawa za kiroho hapa ninashughulika na tiba ya roho!"

Hiyo ndiyo ilikuwa falsafa iliyotawala maisha ya daktari huyu mwenye tabasamu usoni na maneno laini, Dokta Iddi Ibrahim Mwanga aliyetutoka na kutuachia majonzi makubwa tarehe 07/12/2020 na hatimaye kuzikwa na umati wa watu tarehe 09/12/2020 katika makaburi ya Ahmadiyya yaliyoko Wailesi Temeke na sala ya jeneza ikiongozwa na Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Tanzania Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry sahib. Kwa hakika sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.

Iddi Ibrahim Mwanga alizaliwa tarehe 28 Oktoba katika kijiji cha Ugweno, mwaka ule ule lilipozaliwa taifa la Pakistani 1947. Toka darasa la kwanza Iddi Ibrahim Mwanga alionesha bidii kubwa ya masomo. Hakuwa na maskhara hata kidogo na masomo yake. Kutokana na bidii hiyo alijiunga na shule ya Sekondari Tanga alikosoma toka kidato cha kwanza hadi cha sita. Ni wakati yuko shule ya Tanga alipojiunga na Jumuiya ya Ahmadiyya...



Dokta Iddi Mwanga (kushoto) katika mahojiano na aliyekuwa Mhariri wa gazeti hili na mwandishi wa makala hii Mahmood Hamsin Mubiru

Maelezo yataendelea toleo lijalo InshaAllah

Tanzania Yampoteza Mpiganaji



Na Rajabu Mkieti
Ikwiriri, Rufiji

Akilihutubia Taifa saa 5:00 usiku wa machi 17 ,2021.Makamu wa Raisi wa Tanzania alitoa taarifa ya msiba mkubwa kwa Taifa, alisema "Tumempoteza kiongozi wetu shupavu ,Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ,Mheshimiwa Dk John Pombe Magufuli" Hakika ni msiba mkubwa kwa nchi yetu Innallilah wainailahi rajiun (Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea).Hizi ni taarifa nzito zilizotia simanzi kwa taifa na mimi ndipo nilipo nilipokumbuka shairi la Al habibi Muhenga Al ustadhi Khamis S.S. Wamwera katika shairi lake la SIKU YANGU linalosema :-

Wako wapi maasumu, manabii wake mungu
hawana dhambi sehemu, nadhifu kila kifungu
ah! Wote marehemu, nani abaki mwenzangu
ninasema ipo yangu, siku iliyoadhimu

Pale wafalme kemu, na maraisi vipingu
wakitatuwa magumu, na kudhikisha wenzangu
Ah! Nao marehemu, wametunguliwa tengu
Haikosi ipo yangu, siku iliyoadhimu

Siku yangu anayoisema Al habibi Wamwera hasa ni siku itakayomkuta mtu yoyote siku ya umauti, ni kama alivyo inadi yeye mwenyewe na kuiita siku iliyoadhimu.Ama kwa hakika siku hiyo imemkuta aliyekua Raisi wetu Mh. Dk John Magufuli.

Endelea uk 10

Bustani ya Washairi

DUA KWA MAMA SAMIA

1. Ewe Fundi wa kuumba, Mungu tunakulilia
Imara Usiyeyumba, Hujawahipo kosea
Mlezi wa hii nyumba, nchi yako Tanzania
Kwa unyonge twakuomba, mlinde Mama Samia

2. Hiki kipindi kikali, hatujapata pitia
Wanadamu tu dhalili, tufanye kunyenyekea
Tuweke kwenye kivuli, Unachokipendelea
Mungu kwa yako fadhili, faraja awe Samia

3. Mungu ni Yako amri, kila kinachotokea
Mama mpe ujasiri, mazito kuvumilia
Taifa lijaze kheri, kwa udugu kuchanua
Mlinde na kila shari, awe salama Samia

4. Ewe Mungu tuliwaze, misiba ilotujia
Viumbe nini tuweze, bila kutusaidia
Mema ayaendeleze, na malengo kufikia
Mbeleyo umsogeze, Umnusuru Samia

5. Hili ni kubwa jukumu, Mungu ulompatia
Mpe sifa maalumu, za mambo kupangilia
Iimarike nidhamu, askari na raia
Isiishe yetu hamu, utiifu kwa Samia

6. Wangapi akinamama, uliowasaidia
Imara wakasimama, nchi zao kuokoa
Zama zao zikavuma, vilele zikapepea
Mungu kwa zako rehema, fanya kwa mama Samia

7. Mungu mpe usikivu, kwa sifa Yako SAMI'A
Mpambe uvumilivu, nchi kuitumikia
Ukuze wake werevu, aishangaze dunia
Taifa liwe na nguvu, ashinde Mama Samia

8. Yakuze yake maono, kama mama anolea
Malkia wa mfano, kwa nadra kutokea
Aukuze Muungano, asije wa kubomoa
Mungu mshike mkono, Umuongoze Samia

9. Asichague sahiba, mbawa kuwainikia
Tukajapata uhaba, usawa wa jinsia
Mungu uzijaze huba, nyoyo za Watanzania
Wasome akinababa, Mwalimu awe Samia

10. Mungu tunakulilia, hali zetu angalia
Iwe kutubarikia, kutupatia Samia
Ibariki Tanzania, Bara, Visiwani pia
Ibariki Tanzania, Na Umlinde Samia

Sheikh Abdulrahman Mohammed Ame
Dar es salaam

BABU (COMRADE)

1. Nakuomba Rahmani, nisijinasibu sana
Kiburi cha kazi gani, naomba tena na tena
Maringo nayo ya nini, hata nikiitwa bwana
Mwendo umeumaliza, pumzika kwa amani.

2. Kwa wale wakigamboni, wanakufahamu sana
Uliwafundisha dini, ulihubiri mchana
Nisiseme mimi nani, nangu nnipilikana
Mwendo umeumaliza, pumzika kwa amani.

3. Ulisikiliza sana, rafiki wa kila rika
Wala haukujivuna, na mengine kadhalika
Haukuwahi kununa, kila muda ulicheka
Mwendo umeumaliza, pumzika kwa amani.

4. Msomi wa zama hizo, mkali wa hisabati
Ngeli nilikupa tuzo, kwa matamshi ya noti
Ulichukia uozo, kwenye zako harakati
Mwendo umeumaliza, pumzika kwa amani.

5. Uwapo barabarani, na mwendo wa pole pole
Ukifika jamatini, haupendi makelele
Ninakumbuka jamani, sio kwa upole ule
Mwendo umeumaliza, pumzika kwa amani

6. Ulipenda sana dini, ulipapenda kitonga
Ulitii akilini, kwa ukweli hukutunga
Dunia ya kazi gani, jamati ukajiunga
Mwendo umeumaliza, pumzika kwa amani.

7. Ulipokua masasi, cheo chako cha kigogo
Haukufanya uasi, kazi haikua ndogo
Shauri yetu na sisi, vijana wadogo dogo
Mwendo umeumaliza, pumzika kwa amani.

8. 'Liheshimu kila mtu, ili upate jifunza
Haukua Mungu mtu, siri zetu ulitunza
Hukushikiwa mtutu, sala ulizitimiza
Mwendo umeumaliza, pumzika kwa amani.

9. Uliponisalimia, ulijawa na mapenzi
Kidali 'linipatia, 'liniganda kama nzi
Najikaza sitalia, 'linionesha mapenzi
Mwendo umeumaliza, pumzika kwa amani.

10. Tusiwe wapashikuna, kuzisambaza habari
Mfano wa babu hakuna, alitutunzia siri
Haipendezi kununa, wala kuwa na kiburi
Mwendo umeumaliza, pumzika kwa amani.

11. Nisije ongea sana, nakukumbuka salani
Babu yangu ubwa tena, umeondoka jamani
Tutaja onana tena, tutakutana mbeleni
Mimi! Mimi! Mimi! Mimi!, nakumbuka mengi sana.

Abdallah Kalindima
#CHUMACHAKAVU
Wailesi

RAMADHANI INAKUJA

Bisimilahi awali, awali Yake Jalali
Napenda niyasaili, mpate kuyakariri
Muyashike kwa akali, hali zetu kubadili
Ramadhani inakuja, jiandae tafadhali

Ramadhani inakuja, Waisilamu tufunge
Usiache kwa ujanja, kwa kumuasi Jalali
Ukafanya huna haja, ukiumwa na musuli
Ramadhani inakuja, jiandae tafadhali

Tujiandae hakika, tufunge kikwelikweli
Tupate kufarijika, kwa mapenzi ya Jalali
Hii nguzo ya Rabuka, isitukose muhali
Ramadhani inakuja, jiandae tafadhali

Na ulopita wajua, tulifunga kwa akali
Mwaka huu ninajuwa, tujitahidi kusali
Ukiziweza na dua, Manani Akusaili
Ramadhani inakuja, jiandae tafadhali

Ubora wa Ramadhani, hukujenga kiakili
Ukamjua Manani, kwa maombi ya kusali
Tujitahidi jamani, na tusimwasi jalalai
Ramadhani inakuja, jiandae tafadhali

Terehe saba ya Juni, mwaka wa kumi na tisa
Usitadhi wa Khamisi, maombi aliyagusa
Muumba wetu Kudusi, Aiondoe mikasa
Ramadhani inakuja, jiandae tafadhali

Ramadhani ya mwakani, tujaliwe kuigusa
Kwa fadhila za Manani, huenda tukaigusa
Na sasa i karibuni, Allah Tujalie hasa
Ramadhani inakuja, jiandae tafadhali

Kila la heri natoa, nakutakieni mazuri
Muifunge kwa hisia, ya kumjua Manani
Shida zenu mkitoa, kwa kumlilia Jalali
Ramadhani inakuja, jiandae tafadhali

Hapa ndugu kituoni, naweka chini penseli
Hayo yangu yathamini, uyapunguze makali
Umpende na Manani, Akufutie makali
Ramadhani inakuja, jiandae tafadhali

Harun R. Bundala
S.L.P. 54, Kiloleni Bomba Mzinga
Tabora

HAPO UMEPATA MKE

1. Katika ishara zake, Mola wetu Subuhana.
Ni kutuumbia wake, Wake wa kila aina.
Kusudi tupumzike, Tulizo lilo mwanana.
Kama ana sifa hizi, hapo umepata mke.

2. Hatoki bila kuaga, Hata ukiwa safari.
Hana mambo ya kuiga, Ya kumuudhi Kahari.
Na wala hapigi soga, Mambo yazuayo shari.
Kama ana sifa hizi, Hapo umepata mke.

3. AnakufIchia siri, Kwa watu akuhifadhi.
Si fedhuli si jeuri, Ana sitaha na Hadhi.
Sio mwingi wa habari, Kukuletea MARADHI..
Kama ana sifa hizi, Hapo umepata mke.

4. Umpacho huridhika, na dua kukuombea.
Hana mkono birika, ana moyo wa kutoa.
kwa wema anasifika, kila anapotokea.
Kama ana sifa hizi, hapo umepata mke.

5. Hapazi sauti yake, pindi anapo ongea.
Hijabu ni vazi lake, Humkuti kalivua.
Qurani kitabu chake, kutwa anajisomea.
Kama ana sifa hizi, hapo umepata mke.

6. Sala tano anasali, Tahajudi kadhalika.
Na sunna zake Rasuli, Zote kwake kazishika.
Si nahari si laili, Amdhukuru Malika.
Kama ana sifa hizi, hapo umepata mke.

7. Mali ya mume hafuji, Huitunza kama mboni.
Mumewe humfariji, Hali navyokua duni.
Huyo ndo mke "zawwijji" Alitajwa na Manani.
Kama ana sifa hizi, hapo umepata mke.

8. Kama hana hata moja, sifa nilizoandika.
Si mke huyo Kiroja, Atakutia wahaka.
Sasa nini unangoja, Ewe baba ewe Kaka.
Kama ana sifa hizi, Hapo umepata mke.

Twahir Mubiru (Baba Ummybakri)
Dar es salaam

JIUNGENI NAMI

Mie jua la Baraka, Sayari nizungukeni
Na kwenu sina Mipaka, Mpatapo nizuruni
Na msipo bahatika, Kwa barua sabahini
Kwa waso elimika, Niwekeni sujudani
Ni sauti iitayo, Upande wa Ukhalifa

Shunda Mshudia wana
Daluni, Tanga

DAWA NENDA KWA MOLAO

Mambo yakikulemea, usipoteze wakati
Kutwa kiguu na njia, kwa wale wasaka noti
Si waganga nakwambia, haja yao sharubati
Dawa nenda kwa Molao, upate tiba kamili

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani - Migombani

TUNZA HESHIMA YAKO

Itunze heshima yako, kuacha jambo fulani,
Usije kuwa kituko, sababu kitu fulani,
Anguka kwa mola wako, utapata auheni,
Muombe sana manani, Akuze yako imani.

Muombe sana manani, akuze yako imani,
Aepushe mitihani, usiwe majaribuni,
Jambo baya libaini, usipoteze imani,
Itunze heshima yako, Kuacha jambo fulani.

Kalamu naweka chini, kauli yangu natoa,
Naomba uwe makini, katika kila hatua,
Bado upo safarini, mzigo hujautua,
Itunze heshima yako, Kuacha jambo fulani.

Saliana Ramadhani Higiro

Hadithi ya Mchoraji

Palikuwa na mchoraji mmoja ktk moja ya mji mchoraji huyo alikuwa mwenye umri wa utu uzima.

Alikuwa akichora picha nzuri sana na akiziuza kwa gharama kubwa sana.

Siku moja wakamjia maskini na mafukara wa ktk mji ule wakamwambia.

"Wewe unatengeneza kipato kikubwa sana kwa kazi yako hii ni kwa nn hutaki kutusaidia sisi watu wa hali ya chini,,,,,

Watazame wenzako wanaouza nyama ijapokuwa hawana kipato kikubwa lkn kila siku hutoa vipande vya nyama kuwasaidia wasiojiweza."

Mchoraji hakuwajibu chochote ila aliwaonyeshea uso wa furaha tu.

Wale mafukara wa mji ule waliondoka wakichukizwa na suala lile la mchoraji.

Ikawa wakitangaziana pale kijijini kuwa mchoraji yule m/mungu amemjaalia kipato lkn ni mbahiri si mwenye kuwasaidia wasiojiweza.

Baada ya muda mchoraji yule alianza kuugua lkn hakuna mwanakijiji yeyote aliye kwenda kumuona mpk akafa.

Baada ya kufa yule mchoraji siku zilipita na ikawa wale wauza nyama hawatoi tena nyama kwa ajili ya kuwasaidia wasiojiweza.

Wale wanakijiji ikabidi wawaulize wale wauza nyama ni kwa nn hawawasaidii tena nyama kama zamani.?

Wauza nyama wakawajibu kuwa mchoraji alikuwa akiwapa pesa kila mwezi kwa niaba ya kuwanunulia nyama wasiojiweza.

Na wawape bure kila siku lkn alipofariki likasimama jambo hilo kwani hazikutoka tena pesa za kuwanunulia wao nyama kwa kuwa mchoraji ameshakufa.....

• • • •

Keki ya Pundamilia (maarufu zebra)

Na **Mtandao**









Mahitaji

- Unga 1/4, ongeza kikombe kimoja utakacho pimia maziwa
- Siagi 1/4
- Sukari 1/4
- Vanilla kjk 1
- Baking powder kjk1
- Cocoa powder/chocolate paste vijiko 2.
- Maziwa 1/2 kikombe
- mayai 3 au 4

Maelekezo

-

Chukua bakuli lako na utie siagi na sukari, changanya vizuri siagi na sukari. kisha anza kutia mayai.

- Tia mayai huku ukiendelea kuchanganya vizuri mpaka upate mchanganyiko vizuri kisha tia vanilla upendayo.
- Weka unga na upate mchanganyiko laini na unaweza weka maziwa kisha tia baking powder.
- ukishanganya vizuri chukua bakuli lingine na ugawe sawa mchanganyiko nusu kwa nusu.
- Chukua cocoa au chocolate paste weka kwenye mchanganyiko wa bakuli moja changanya vizuri.

◎Andaa Sufuria ya kuokea paka siagi na unyunyizie unga kisha ,,,,

◎Anza kuweka kwa tumia kijiko au mimina chota kdg kdg anza na mweupe kijiko kimoja halafu weka wa cocoa kijiko kimoja. fanya hivyo mpaka utakapomaliza kwa kupokezana

ASEMAVYO MASIHI ALIYEAHIDIWA AS

Shabaha za Kuanzishwa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

Enyi marafiki zangu mliofanya maagano nami, Mungu Aniwezeshe na Awawezesheni kutenda yale yatakayompendeza Yeye. Leo hii ninyi ni wachache katika idadi. Mnapita katika kipindi chenye majaribio makubwa. Sawa na kanuni Zake za azali, ilikwisha ridhiwa na Mwenyezi Mungu tangu kale kwamba juhudi zitafanywa toka kila upande ili ninyi mteleze. Mtasumbuliwa kwa kila njia, nanyi mtalazimika kuvumilia matamshi ya kila aina. Kila mmoja wa wale watakaowataabisheni kwa ulimi wake ama kwa mkono wake, atafanya hivyo akiamini kwamba anaihudumia Islam. Hali kadhalika, mtatahiniwa mbinguni ili kwamba muwe mmetahiniwa kwa kila njia iwezekanavyo. Fahamuni kwa hivyo, ya kwamba njia ya ushindi kwa ajili yenu haielekei kwenye hoja kame mtakazotumia au kwamba ninyi muwazomee wanaowazomeeni au kwamba myajibu matusi kwa matusi. Mkitumia mbinu hizi nyoyo zenu zitakuwa kavu nanyi hamtabaki na cho chote ila maneno matupu ambayo Mwenyezi Mungu Anayachukia na kuyabeza. Hivyo basi, msishike tabia ambayo kwayo zitahakiki juu yenu laana mbili - laana ya watu na laana ya Mungu.

(Roohani Khazain Jal. 3 Uk. 546-548; Azala-e-Auhaam Uk. 446).

DARASA LA QUR'AN TUKUFU

UMUHIMU WA SALA ZA JAMAA

Na **Musa Salum Mgeleka -** 0717 504 690

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا نُودِيَ لِلصَّلَاةِ مِنْ يَوْمِ الْجُمُعَةِ فَاسْعَوْا إِلَىٰ ذِكْرِ اللَّهِ وَذَرُوا الْبَيْعَ ۚ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ)

Enyi mlioamini! Inaponadiwa kwa ajili ya Sala ya siku ya Ijumaa, basi nendeni upesi kumkumAbuka Mwenyezi Mungu na acheni biashara; hiyo ni bora kwenu ikiwa mnajua. [Surat Al-Jumu›ah 10]

SALA YA IJUMAA Imefaradhishwa moja kwa moja Kusaliwa kwa Jamaa. Umuhimu huo huoenea na kupatikana kwa kila Sala za Faradhi zinapo saliwa kwa Jamaa. Sala ya Jamaa husaliwa pamoja ambapo Imamu na Mamuma huwepo na Mistari pia huwepo. Katika Mazingira kama haya watu wa aina mbalimbali Uchamungu, waovu, Masikini na Matajiri hukutanishwa pamoja. Imamu huongoza Sala na Mamuma hupaswa Kufuata na Kutii kila Kitendo cha Imamu bila Kumtangulia jambo lolote.

Kunamanufaa 27 yatokanayo na Sala ya Jamaa. Kama Mtume*saw* alivyosema kuwa Sala ya Jamaa inadaraja zaidi mara 27 Kwa Sala ya Binafsi. Leo nitaeleza manufaa machache sawa na wasaa niliojariwa kuyafahamu, Inshaallah

Sawa na Tabia za Asili za Mwanadamu, Tabia moja huweza kuhama bila kupunguza, kufutika au kuambukiza kwa mwingine kwa njia ya Kugusana. Kuna Hadithi ya Mtume*saw* Inayosema Chuki zenu huondoshwa kwa Kunyosha Mistari kwenye Sala na Sehemu nyingine Anasema Enezeni Desturi ya Kusalimiana kwa kushikana mikono itaondosha Chuki baina yenu na Pia kuna Sehemu ya Anasema unapoenda Kumjulia hali mgonjwa Msalimie kwa Kumshika Mkono au Paji la uso (hapa sinakumbuka vyema ni mkono au paji la uso). Pia Mtume*saw* alisema kuwa kukiwa na Nafasi baina yenu kwenye Mstari wa Sala baina ya mtu na mtu basi nafasi hiyo ni ya shetani baina yenu. Ilimradi Desturi ya kugusana ina maana sana kimwili na Roho. Ndivyo Sala ya Jamaa ikawekewa umuhimu wake mbalimbali.

1◎ Nidhamu ya juu kabisa ya UTII inapatika. Ambapo kila mmoja hutii Amri za Imamu mmoja apende asipende. Na desturi hii huambukizwa kwa kila mmoja wake atakaye dumisha Sala za Jamaa.

2◎ Sala ya Jamaa Hufuta Madhambi (Kusamehewa Makosa) na Kupandisha Madaraja ya Wema na Uchamungu. Hadithi ya Mtume*saw*. Kuna Sahaba Alifanya Kosa na akafika kwa Mtume*saw* ili apewe Adhabu sawa na Kosa lake na muda wa Sala ulikuwa umewadia, walisali kisha yule Sahaba akaomba apewe Adhabu, Mtume*saw* akasema hatukusali pamoja? Umekwisha Samehewa kwa Kusali Sala ya Jamaa.

3◎ Masih Aliyeahidiwa*as* Anasema Sala ya Jamaa hueneza Umoja. Kila Binadamu ana Fundo lake na ndivyo Mtume*saw* anavyosema kila siku Mtu huamka na mafundo 360 asipoomba Maghofira na Kutenda Wema Sawa na idadi hiyo basi mafundo huendelea kumsumbua. Masih Aliyeahidiwa as Anasema Mwanadamu huwa na Mafundo na Ubinafsi ni Sala ya Jamaa tu ndio huyaondoa. Umoja na Upendo hupatikana ikiwa mafundo na ubinafsi wenu yakitoka vinginevyo chuki, Dhuluma, uuwaji na Uwongo huenea baina yenu.

4◎ Rahisi kupokelewa Dua. Masih Aliyeahidiwa as anasema; Allah hupenda Dua inayoombwa pamoja na kwa wingi. Kwenye Eid el Fitri ya Mwaka Jana Khalifatul Masih V atba Alisema Kusali Sala tano kwa Wakati wake na Nafali na Witri Neno Alhamdulillah linaombwa mara 40 kwenye Sala. Ambapo kwenye Sala ya Jamaa Neno hili hutamkwa mara nyingi zaidi ya 40 kwenye Sala moja na kufanya Maombi yenu kupokelewa. Na Mtume*saw* Alisema Muombeeni Maiti na ikiwa Sala yake imesaliwa na watu 100 na Sehemu nyingine 40 Maombi yenu juu Maiti hupokelewa. Haya yote yanaonyesha umuhimu wa Sala ya Jamaa.

Maombi mengi watu wakilalamika hayapokelewi ikiwa pia nao hawasali Sala za Jamaa na hata nyuma ya Wachamungu.

Khalifatul Masih V*atba* Kuona Umuhimu wa Sala za Jamaa Akawashauri Wanajamaat anagalau Sala mbili kwa siku wakajitahidi Kusali Sala za Jamaa na Kuzingatia Kusali Sala zote Sawa na nyakati zake zilizopangwa. Kuchanganya iwe dharula na akaonya Desturi iliyojengeka ya kila siku kuchanganya Sala za Adhuhuri na Alasiri na Magharibi na Ishaa kiasi hiki maana ya Sala tano sasa inajulikana ni Sala tatu.

Tunamuomba Allah Atujalie tuwe wenye kusimamisha Sala kwa Nyakati zake na Kutufanya Kusali Sala za Jamaa. Amin

MATUKIO KATIKA PICHA





Khuddamul Ahmadiyya wa tawi la Ushetu wakifanya Wakal Amal katika Zahani ya Uyogo huko Kahama, Shinyanga





Darasa la Atfal na Nasrat Mwanza. Kulia ni picha ya pamoja baada ya darsa na Sheikh wa Mkoa na baadhi ya wanajamaat. Kushoto ni darsa likiendela



Picha ya pamoja wa wanajamaat wa Zanzibar baada ya maadhimisho ya Siku ya Mwana Aliyeahidiwa[as]



Ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya mkoa wa Dar es salaam baada ya kusaini kitabu cha rambirambi ya Hayati Dr. John Pombe Magufuli



Ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya mkoa wa Shinyanga baada ya kusaini kitabu cha rambirambi ya Hayati Dr. John Pombe Magufuli



Ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya mkoa wa Arusha baada ya kusaini kitabu cha rambirambi ya Hayati Dr. John Pombe Magufuli

Tanzania Yampoteza Mpiganaji

Kutoka uk. 5

Msiba huu umekuwa mkubwa na kutia simanzi kwa Taifa japokuwa Tanzania imewahi kupata misiba ya viongozi wa kitaifa lakini mara hii ni ya kwanza katika historia ya nchi yetu ikimpoteza Raisi aliyeko madarakani.Hayati Dk John Magufuli alizaliwa oktoba 29,1959 siku ya Alhamis katika kijiji cha katona kata ya Bugando,Tarafa ya Nzela,wilaya ya Geita wakati huo.Wazazi wake ni Magufuli Marco Nyahinga na Bi Suzana Musa ambao kati ya 1961 waliamua kuhama kuvuka ziwa Victoria (Lweru) kutoka Katoma Nkome, wilaya ya Geita, Mkoa wa Mwanza wakati huo, kwenda kijiji cha lubambangwe,Chato wilaya ya Biharamuro Mkoa wa Kagera wakati huo,kutafuta fursa za kiuchumi. Mwaka 2012 Serikali ya Tanzania ilifanya mabadiliko na kuanzisha mkoa mpya iliyoiondoa Chato katika Mkoa wa Kagera na kuileta katika mkoa mpya wa Geita.Familia ya Hayati Dk John Magufuli ilikua ni familia ya kawaida kabisa ya wakulima na wafugaji,yeye malezi na maadili mema,ni familia ilikua na ari na utashi katika kujituma kuchapa kazi kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.Hali hii ndio iliyo mfanya mwana wao katika familia kijitoma katika siasa mwaka 1995 na kushinda kiti cha ubunge katika jimbo la Biharamuro mashariki wakati huo kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM). Aliwahi kushika nyazifa za uwaziri katika awamu ya Tatu ya Raisi Benjamin Mkapa na Awamu ya Nne Raisi Jakaya Kikwete ambamo katika nyakati zote zilimfanya apambanuke kuwa ni mtu mchapakazi na mahiri katika kazi zake na mwenye kufanyaa bidiii milithili ya mchwa. Mwaka 2015 wana Chato pamoja na Watanznania ilikua ni baahati na nderemo kwa kipenzi chetu Dk Magufuli baada ya kushinda kiti cha Uraisi na kuwa Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzani kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM),Alipo shika kiti cha urais mambo ndio yalipamba moto kwani hakuwa tena lelemama aliongezajuhudi na bidii katika kazi alijipambanua kuwa ni mtetezi wa wanyonge kwa kusimamia rasilimali za Taifa na kutaka zisaidie Taifa zima, halii ilimfanya watu wengi wampenda na kumsaidia katika kazi zake za uraisi. Hayati Raisi Magufuli katika maisha yake hakuwa na usiku wala mchana wakupumzika alijifunga mkanda kuhakikisha Watanzania wanapata maendeleo alianzisha miradi ya kimkakati yenye maslahi makubwa kwa Taifa baadhi ya miradi hiyo ni maradi wa reli ya kati SGR, Mradi wa bwawa la kuzalisha umeme katika mto Rufiji,kuongeza upatikanaji wa vituo vya afya pamoja na hospitali,katika hali hiyo ndipo ilidhihirika sifa yake ya kuwa mpambanaji na mpiganaji wa maslhi ya Taifa na Afrika alipenda miradi yote ya kimkakati kufadhiliwa kwa fedha za ndani ya nchi na hakupenda mikopo kutoka nje ya nchi kwani masharti yake ndio yalikua hayana maslahi mapana kwa Taifa. Mwaka jana 2020 aliingia katika kinyanganyiro cha uchaguzi na kubahatika kushika tena kiti cha urais, kwa mapenzi ya Mwenyezi Mungu 17 machi 2021 aliagadunia Innalillahi wainaillah rajiuni (Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea).Katika kumuelezea Hayati Rais Magufuli viongozi wanchi mabali walimueleza kua alikua ni kiongozi mahiri na mwana mwema wa afrika aliyeipenda kwanza Afrika na nchi yake.Hayati Raisi magufuli atazikwa nyumbani kwao chato 26/03/2021.



Hayati John Pombe magufuli baada ya kuapishwa kuwa Rais mwaka 2015

Masahaba Walioongoka: Hadhrat Uthman[ra]

Kutoka uk.11

akienda msikitini peke yake. Hata wakati alipokuwa amefungwa nyumbani kwake, aliwaamuru Maswahaba[ra] warudi nyumbani, badala ya kukaa naye ili kumlinda. Hata waasi walipoingia nyumbani kwake, aliendelea kusoma Qurani Tukufu bila woga wowote. Halafu, hata wakati mtoto wa Hazrat Abu Bakr[ra] aliposonga mbele kumshambulia, aliweza kumsaidia kwa utulivu kumuonesha ubaya wa kitendo chake. Kwa hiyo, matukio yote yaliyosababisha kuuawa kwake kwa hakika yanaonyesha wazi kuwa yeye Hazrat Uthman[ra] hakuwa na hofu yoyote hata kidogo.

Khalifa Mtukufu[atba] alisema baada ya kuuawa kwa Hazrat Uthman[ra] ndipo watu walipoanza kuelewa umuhimu wa kweli wa Khilafat. Khalifa Mtukufu[atba] aliendelea kuelezea fadhila za ajabu alizo nazo Hazrat Uthman[ra]. Khalifa Mtukufu[atba] alielezea hadhi yake tukufu, na kwamba hata Mtukufu Mtume[saw] alimheshimu sana. Kwa mfano, wakati mmoja, Mtukufu Mtume[saw] alikuwa amelala chini, na Hazrat Abu Bakr[ra] aliingia, lakini Mtukufu Mtume[saw] aliendelea kujilaza. Kisha Hazrat Umar[ra] akaingia lakini Mtukufu Mtume[saw] aliendelea kujilaza. Kisha Hazrat Uthman[ra] akaingia, na Mtukufu Mtume[saw] mara moja akaanza kurekebisha nguo zake, na baadaye akasema Hazrat Uthman[ra] ni mtu mwenye unyenyekevu mkubwa, Mimi nimefanya hivi kwa kuzingatia hisia zake za kuona haya. Hazrat Uthman[ra] alikuwa mmoja wa wale watu sita ambao Mtukufu Mtume[saw] aliwatabiria daraja la juu la ubora, na alikuwa mmoja wa wale masahaba kumi ambao Mtukufu Mtume[saw] aliwatabiria Janna (pepo).

Khalifa Mtukufu[atba] alisema ataendelea kuangazia matukio ya maisha ya Hazrat Uthman[ra] katika hotuba za Ijumaa zijazo.

Tanzia:

Khalifa Mtukufu[atba] alitangaza misiba ya wanajumuiya wanne waliofariki hivi karibuni.

1. Maulvi Muhammad Idrees Sahib kutoka Ivory Coast ambaye alifariki usiku wa tarehe 27 na 28 Februari. Alisoma Jamia huko Rabwah, baada ya hapo alipata heshima ya kutumikia kama Mbashiri huko nchini Ivory Coast na nchi zingine mbali mbali. Alikuwa hodari na mwenye bidii katika mahubiri. Alikuwa na mapenzi mkubwa na Jamaat na Ukhalifa, kiasi kwamba kama mtu alimuuliza juu ya utaifa wake alijibu yeye ni mwahmadiyya. Ameacha nyuma mke, mabinti wanne na mtoto wa kiume. Khalifa Mtukufu[atba] aliomba kwamba watoto wake waweze kufuata nyayo zake na Mwenyezi Mungu amuinue mahala pake Peponi.

2. Amina Nayga Kare Sahiba ambaye alikuwa mke wa Amiri wa Jumuiya nchini Uganda. Alifariki mnamo Februari 20. Alikuwa mtaalamu na mwenye elimu kubwa, Alikuwa na shauku kubwa ya mahubiri. Ameacha nyuma mumewe na watoto sita, ambao kati yao wawili ni wabashiri.

3. Noohi Kazak Sahib aliyefariki mnamo Desemba 10, 2020. Alikuwa mcha Mungu sana, yeye alikuwa ni mwenye kusali sala zote. Alikuwa na mapenzi makubwa na Ukhalifa. Ameacha wake wawili na wasichana wadogo watatu. Siku zote alikuwa tayari kuitumikia Jumuiya kwa uwezo wowote na hali yoyote inayohitajika. Alikuwa mkarimu kwa wengine. Badala ya kujikusanyia utajiri, alikuwa anawasaidia wale waliokuwa wanahitaji. Mmoja wa kaka zake anayeitwa Mutaz Kazak Sahib, ni Mhadhiri huko Jamia Ahmadiyya Canada.

4. Farhat Naseem Sahiba wa Rabwah, nchini Pakistan aliyefariki mnamo Desemba 26, 2020. Alikuwa mcha Mungu sana, alikuwa anasali sala zote. Alikuwa anawasaidia maskini, na mwenye kutoa michango mfululizo. Ameacha watoto watatu wa kiume, na watatu wa kike na wajukuu wengi. Mmoja wa wanawe na wajukuu zake wawili ni wabashiri. Khalifa Mtukufu[atba] aliwaombea hawa wote rehema na msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na kuinua daraja lao peponi.

Kwa nini Biblia Ni Jibu Wanamkana Nabii Issa kuwa Si Yesu?

Inaendelea Kutoka toleo lililopita

HOJA YA TATU

Majina na maana yake na asili yake, Maana ya jina Issa na maana ya jina Yesu .Kama ita onekana mambo hayo yaliyo onekana hapo juu wote wanayo ama wamehusika basi basi atakuwa ni mmoja na tofauti itakuwa ni majina kama wanavyo sema kwa mfano kama itaonekana maana ya majina ni ileile basi Isa atakuwa ndie Yesu na ikiwa tofauti basi watakuwa wawili tofauti (kwa kiarabu Thinani mutatarikani)

MAJINA NA (Maana yake ya asili)

ISA- Maana yake ni wekundu uliochanganyika na weupe (Albino au Zeruzeru)kwa hiyo Isa ni jina la kiarabu ushahidi huu upatikana katika tafsiri ya Imamu Baidhaw vol:ukurasa 160.

YESU- Jina la yesu lilikuwa jina la kawaida la kiyahudi nalo linaonekana katika lugha ya kiyunani kwenye agano jipya likiwa sawa na jina la Yoshua la Kibrania katika Agano la kale . Maana ya jina hilin ni Yahuew (Yehova) ni mwokozi wetu hivyo lilitoa kuwa jina kwa yeye ambae ange okoa watu wake yani watun wa Yahieh kutoka dhambi zao-mwisho wa kunukuu halafu akanza tena mwandishi wa biblia ni jibu :

Tusomapo katika Injili ya M.t 1:18-21 Bibilia ya kiarabu inasomeka hivi – *AMMA WILADAT YASUA L- MASIH takqnat hakadhaa Iamma Koanat Maryamo , Ummuhu Makhoobatan Liyusufu kabla ya Qudus* yani kuzaliwa kwake Yesu kristo kulikuwa hivi Mariamu mama yake hawajawa karibiana alionekana ana Mimba nae atazaa mwana nawe utamwita jina lake Yesu maana yeye ndie atakaye waokoa watu wake na dhambi zao.

Waandishi wanasema huu ni ushahidi wa kwanza juu ya utofauti wa ISSA na Yesu kwa sababu maana ya Issa ni WEKUNDU ULIOZIDIANA NA WEUPE WA MANJANO.

Na maana ya jina la YESU MWOKOZI . Ingawa watu husema kuwa jina ni lilelile lakini tofauti ni lugha akimaliza hoja yake. Anasema hii si kweli kwa sababu jina la Yesu ambalo Maana yake ni Mwokozi hata likibadilika katika lugha bado maana hubaki kuwa ileile ya Mwokozi na tutatoa baadhi ya lugha wana mwitaje mfano KIYUNANI yesu. KIARABU – yasua , KINGEREZA JESUS KISWAHILI Bwana anaokoa mwisho wa kunukuu.

Ukweli Inasikitisha pale mwandishi wa Biblia ni jibu anapoanza kutoa tafsiri isiyo kwa halali akimaanisha wekundu uliochanganyika na weupe akasema (ALBINO –AU ZERUZERU)Wakati sio sifa ya neon hilo. Nahisi itakuwa tabia ya unyanyapaa basi Mwandishi huyu juu ya jamii hiyo ya Albino lakini Mwandishi ajue hata albino ni watu na kama sio unyanyapaa basi Mwandishi huyo anajua jinsi wachungaji waliopewa karama ya maombi ya kuponyesha walemavu walivyo kwama kuwa ponesha walemavu wa ngozi kuwa na ngozi Imara kama wao.

Issa ni wekundu wa manjano uliochanganyika na weupe cha msingi ni kutaka kujua. Sifa hiyo inaingia vipi kwa Yesu? ni kwamba kwa asili hiyo ni sifa ya viumbe ambavyo mayai yake hayapandwi au kuatamiwa. Maana yai lenyewe wekundu uliochanganyika na weupe hata lingekuwa la kuku maana tayari utakuwa umepevuka na halikaangwi tena hivyo kwa mujibu wa maandiko kuna swali aliuliza Mariyamu mama yake Yesu. Quran sura 19:21 Akasema ninawezaje kupata mtoto hali haja nigusa mwanaume yeyote wala mimi si Asherati? Hapo ndipo asili ya jina lenyewe la Issa Maana yake yai lake ni pevu lilo tayari limeshachanganyika na kupevuka hivyo halihitaji mchanganyiko kutoka nje ya umbile lake pamoja na hivyo Jamii ya watu hawa kumuamini Mariamu kama alimpata mtoto huyo yeye mwenyewe . ndipo Quran ikatoa msisitizo katika sura 19:35;

Huyo ndo Issa bin Mariam .Ndiyo kauli ya haki ambayo wanaifanyia shaka .

Yani hilo ndio yai lilo pevuka bil msaada wa mwanaume ila Mariam mwenyewe .ndo ukweli halisi ambao watu wana ufanyia shaka . Hivyo kwa ufupi Issa ni yai lisilo pandwa na wekundu ulio changanyika na weupe ni ukomavu wa kupevuka .

Maana asili ya yai ni weupe ulio na manjano na likalaliwa na kupevuka kabla ya kuzaliwa huja katika hatua ya Issa – wekundu ulio changanyika na weupe hivyo mwandishi angejua ni mfano ya maumbile ya viumbe mbalimbali angekuwa muelewa na asingesema tafsiri ni Albino .

Halafu akasema jina Yesu ni jina la kawaida la kiyaudi nalo linaonekana katika lugha ya kiyunani kwenye agano jipya . Ukweli Yesu sio jins la kiyahudi ila ni jina la kiyunani Wayunani ndio walio mwita Yesu ambalo waebrania walimwita Yeshua swala sio maana ila kwanini YOSHUA halikuvuma na Yesu likavuma ni kwamba walio mwita Yeshua ya waebrania ambao ndo wayahudi wao hawakuwamini kama ni Nabii na nakam alikuwa mtoto halali na Wayunani ambao ni wagiriki ambao wao walimwamini wakadumisha jin hilo lakini wakimaanisha Mtoto wa JOSEPH AU YUSUFU nan doo mzaliko wa Wa Yusuph – Yesu na Joseph –Jesus swala hapo lakusema Yesu ni mwokozi hapo halipo kwani wayahudi walikuwa wanamtegemea ni mtu mwenye cheo cha Masihi ihivyo hata angeitwa simba ulanga kwao isingekuwa tatizo na ndio maana tunasoma . Yohana

Aliwatuma wanafunzi wake wakamuulize kama yweye ndie Masihi au wamsubiri mwingine hata Yohana 1:19:-20; Nauo ndio ushuhuda wake Yohana wayahudi walipo tuma kwake makuhani na walawi kutoka Yerusalem ili wamuulize wewe unani?Nae akakili wala hakukana alikiri kwamba mimi sio Kriston (MASIHI)

Mfano mwingine Yohana 7:41;42 Wengine walisema Huyu ndie kristo (Masihi) wengine wakasema je kristo atatoka galilaya ?Andiko halikusema yakwamba kristo atatoka katika uzao waDaudi na kutoka Bethlemi mji alio kaa Daudi ?niwazi cheo cha Masihi ndio kilikuwa kinangojewa sio jina Yesu au jina Issa.

Itaendelea toleo lijalo

Masahaba Walioongoka: Hadhrat Uthman ra

Kutoka uk.12

Khalifa Mtukufu atba alisema siku ambayo nyumba ya Hazrat Uthman ra ilizingirwa, masahaba wengine pia walikuwepo nyumbani kwake, na wakasisitiza lazima kundi moja la waaminio liwepo ili kumlinda Hazrat Uthman ra dhidi ya waasi. Walakini, Hazrat Uthman ra alisema hakuna haja ya damu ya mtu yeyote kumwagika kwa ajili yake, pia wala mtu yeyote hapaswi kumwaga damu ya mtu mwingine kwa ajili yake.

Khalifa Mtukufu atba alisema kwa njia hii, Hazrat Uthman ra hakutoa nafasi kwa waasi kuhalalisha matendo yao mabaya au kuhalalisha vita dhidi yake na waaminio.

Waasi wamuua Hazrat Uthman ra

Khalifa Mtukufu atba alisema wakati waasi walipoona kwamba kuna Waislamu waliojitolea wamekusanyika kwenye mlango wa Hazrat Uthman ra wakajua kuwa itakuwa ngumu kuingia nyumbani kwake. Kwa hiyo, waliamua kwenda kwenye nyumba ya jirani na kuingia kutoka pale. Walipoingia nyumbani kwa Hazrat Uthman ra, walimkuta akisoma Qur'ani Tukufu. Hazrat Uthman ra alijua kuwa hii ndiyo siku yangu ya kuuawa shahidi, na kwa hiyo akawachagua watu wawili kulinda hazina ya waaminio ili mtu yeyote asiweze kuiba.

Khalifa Mtukufu atba alisema kwanza, mtoto wa Hazrat Abu Bakr ra alisonga mbele, na alishika ndevu zake na kumvuta kwa nguvu. Hazrat Uthman ra akamwambia kama baba yako (Hazrat Abu Bakr ra) angekuwa hai leo usingeweza kufanya haya. Baada ya kusikia hayo, alisogea nyuma na kuondoka. Walakini waasi wengine walisonga mbele, na mmoja wao akampiga Hazrat Uthman ra kichwani na fimbo ya chuma, na damu ikaanza kumtoka kichwani. Waasi, bila kujali chochote, walipiga teke Qur'ani Tukufu ambayo Hazrat Uthman ra alikuwa anasoma. Kwa bahati mbaya, damu ya Hazrat Uthman ra ilianguka kwenye aya ifuatayo:

'Na hakika Mwenyezi Mungu atakulipizia kisasi dhidi yao, kwani Yeye ni Mwenye kusikia, Mjuzi.' (2: 138)

Ndipo waasi wakaendelea kumshambulia. Wakaanza kumkata kwa panga zao. Hazrat Uthman ra alijaribu kuzuia mashambulizi haya kwa mkono ambapo ulikatika. Katika wakati huu, Hazrat Uthman ra alisema huu ndio mkono ambao ulioandika aya za Qur'ani Tukufu mara ya kwanza. Muda ule ule, mke wa Hazrat Uthman ra akaja na kusimama mbele yake, lakini wale waasi hawakusita hata kumshambulia mwanamke, hadi kumkata vidole vyake. Halafu waliendelea kumshambulia Hadhrat Uthman ra mpaka walipomuua shahidi. 'Hakika sisi ni waja wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea.'

Hazrat Uthman ra Aonesha ujasiri

Khalifa Mtukufu atba aliendelea kumnukuu Khalifa wa Pili ra ambaye alilieleza tukio hili na kusema kwamba wakati waasi walipokuwa wakimshambulia Hazrat Uthman ra, walikuwa wakitumia lugha chafu juu ya mkewe, na Zaidi ya hayo, juu ya Hazrat A'ishah ra pia. Walakini pamoja na haya yote, Hazrat Uthman ra hakuogopa kuuawa. Hata hapo nyuma kabla ya haya, alikuwa

Endelea uk 10

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

RAJ.-SHAB. 1442 AH | MACHI 2021 | AMMAN 1400 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu^{saw}

Imesimuliwa na Hadhrat Anas r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah^{saw}. alisema: Alama mojawapo ya Saa ni kwamba watu watajifaharisha katika misikiti. (**Abu Dawud**).

Makhalifa Walioongoka: Hadhrat Uthman^{ra}

Katika hotuba ya Ijumaa ya tarehe 12/03/2021 iliyotolewa Masjid Mubarak, Islamabad, UK; baada ya Tashahhud, Ta'awwudh na Surat Faatihah, Khalifa Mtukufu, Hadhrat Amir ul Mu'miniin, Mirza Masroor Ahmad^{atba} ('Ayyadahullahu Ta'ala Bi-Nasrihil Aziiz') alisema kwamba kuwa ataendelea kuangazia matukio katika maisha ya Hazrat Uthman^{ra}.



Masjid Mubarak: Hadhrat Khalifatul Masih V^{atba} huhutubia Ijumaa kwa waaminio tokea na kurushwa duniani kote kwa njia ya satelaiti.

Mapendekezo ya Amir Mu'awiyyah kwa Hazrat Uthman^{ra}

Khalifa Mtukufu^{atba} alisema Hazrat Uthman^{ra} alifanya Hija yake ya mwisho karibu mwaka mmoja kabla ya kifo chake. Wakati huo, waasi walikuwa tayari wameanza fujo zao. Amir Mu'awiyyah alikuwa amefuatana na Hazrat Uthman^{ra}, na akamshauri Hazrat Uthman^{ra} kwamba aende Syria pamoja naye, kwani machafuko yalikuwa yanazidi kuongezeka. Hazrat Uthman^{ra} alijibu kwamba yeye hawezi kuwa mbali na Mtukufu Mtume^{saw} katika hali yoyote. Ndipo Amir Mu'awiyyah alipendekeza kwamba atume jeshi kutoka Siriya kwa ajili ya ulinzi wa Hazrat Uthman^{ra}. Hazrat Uthman^{ra} akajibu kwamba hatakubali gharama yake itolewe kutoka katika hazina ya waaminio kwa ajili ya ulinzi wake. Ndipo Amir Mu'awiyyah alipoongeza kwamba kama maswahaba hawa watabakia Madina basi waasi watafikiria kuwa tukimuondoa Khalifa Uthman^{ra} mtu mwingine anaweza kushika nafasi yake, kwa hiyo ni bora maswahaba hawa wakawa nje ya Madina ili waasi wasifikirie jambo hili na wewe utakuwa salama.

Hazrat Uthman^{ra} akajibu kuwa hawezi kuwatawanya wale ambao Mtukufu Mtume^{saw} aliwaweka pamoja.

Wakati wa mazungumzo haya Hazrat Amir Mu'awiyyah alikuwa anatokwa na machozi, na akasema kwamba Hazrat Uthman^{ra} anatakiwa atangaze kuwa kama chochote cha hatari kitatokea kwake, basi yeye Amir Mu'awiyyah apate ruhusa ya kulipiza kisasi. Hazrat Uthman^{ra} alijibu kuwa chochote kilichokusudiwa kutokea nakitokee, kwa hiyo yeye hakuweza kufanya hivyo.

Hazrat Uthman^{ra} Awaonya Waasi

Khalifa Mtukufu (aba) alisema wakati Hazrat Uthman^{ra} alipokuwa amefungwa nyumbani kwake na waasi, aliwaambia watekaji wake kwamba hawapaswi kumuua. Alisema kwamba ikiwa watafanya hivyo, hawataweza kusali pamoja baada yake katu, na hawataweza kuungana kamwe katika kupigana dhidi ya adui. Aliwashauri waachane na fujo. Walakini waasi hawakuzingatia maneno yake. Na kwa hivyo, Hazrat Uthman^{ra} alimwomba Mungu, Aweke hesabu ya wale wote waliozingira nyumba yake na kusababisha uasi huu na kuwaadhibu ipasavyo. Inasimuliwa kwamba wale wote ambao walishiriki katika uasi huu hatimaye wote waliangamia.

Endelea uk 11





Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya inaungana na wananchi wote nchini kuomboleza kifo cha Rais wa awamu ya tano Dr John Pombe Magufuli.

Sisi sote ni wa Allah na Kwake tutarejea.

Tunamuomba Allah Adumishe umoja, amani, mshikamano, na mambo aliyoyasimamia kwa nguvu zake zote. Na njia njema na bora ya kumkumbuka ni kudumisha hayo aliyoyathamini na kuyaenzi.

Pia Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya inamuombea Rais wa awamu ya sita Mama Samia Suluhu Hassan msaada kutoka kwa Allah ili aweze kututumikia kwa uadilifu na kuwa kivuli kwa Watanzania wote.

Mungu Ibariki Tanzania

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com